**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAISI**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA**

# KABRASHA LA ZABUNI

**ZA**

**UWAKALA WA USAFISHAJI, UKUSANYAJI NA USAFIRISHAJI WA TAKA NGUMU KWA MWAKA 2022/2023**

**SEPTEMBA 2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA**
**(*Barua zote zielekezwe kwa Mkurugenzi wa Halmashauri*)**

Simu Na. 026 - 2702647
Fax. Na. 026 – 2702203
Email:md.@iringamc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa,
S.L.P. 162,
**IRINGA**

## TANGAZO LA ZABUNI
## ZABUNI ZA UWAKALA WA USAFISHAJI WA MANISPAA

1. Halmashauri ya Manispaa ya Iringa inakusudia kutumia huduma za wakala katika kazi za usafishaji wa mji kwa kipindi cha kuanzia tarehe 01/10/2022.

2. Halmashauri ya Manispaa ya Iringa chini ya utaratibu wa zabuni za ushindani kimkoa (Regional Preference Scheme, GN No 446 ya mwaka 2013 kama ilivyofanyiwa marekebisho) inawaalika watu Binafsi, Makampuni, Ushirika, Taasisi au Vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria, wenye nia na uwezo wa kufanya kazi hizo kutuma maombi ya zabuni za usafi wa mji kama ifuatavyo :

| NAMBA YA ZABUNI | KANDA | KATA | ADA YA ZABUNI (TSHS.) | WANAOSTAHILI |
|---|---|---|---|---|
| LGA/025/2022/2023/N/01<br><br>FUNGU LA 1 | Igumbilo,Ruaha, Kitwiru na Kwakilosa | A | 50,000/= | Makampuni, ushirika, taasisi, vikundi vilivyosajiliwa kisheria, watu binafsi |
| LGA/025/2022/2023/N/02<br><br>FUNGU LA 2 | Gangilonga, Kitanzini, Makorongoni, Mivinjeni na Mshindo | B | 50,000/= | Makampuni, ushirika, taasisi, vikundi vilivyosajiliwa kisheria, watu binafsi |
| LGA/025/2022/2023/N/03<br><br>FUNGU LA 3 | Mlandege, Mwangata, Isakalilo, Mkwawa na Ilala. | C | 50,000/= | Makampuni, ushirika, taasisi, vikundi viliovyosajiliwa kisheria, watu binafsi |
| LGA/025/2022/2023/N/04<br><br>FUNGU LA 4 | Kihesa, Mtwivila, Mkimbizi na Nduli | D | 50,000/= | Makampuni, ushirika, taasisi, vikundi vilivyosajiliwa kisheria, watu binafsi |

**MASHARTI YA JUMLA KWA ZABUNI ZOTE**

1. Nakala ya leseni hai isipokuwa vikundi vya kijamii vilivyoandikishwa, CBO's hazihusiki na sharti hili.
2. Waombaji wote waambatanishe nakala za usajili wa makampuni au vikundi vya kijamii (CBOs).
3. CBOs ziambatanishe orodha ya viongozi wa kikundi na barua za utambulisho toka kwenye kata husika.
4. Waombaji wambatanishe nakala zausajili wa VAT na TIN. isipokuwa CBOs

5. Waombaji wawe na magari yenye hali nzuri na vifaa vya kutosha kukusanya, kupakia na kusafirisha taka kuzipeleka katika dampo.
6. .Mwombaji ni lazima aambatanishe wasifu wa kampuni/mtu binafsi/kikundi (Applicant Profile).
7. Mwombaji ni lazima aambatanishe tamko rasmi la kutokujihusisha na vitendo vya rushwa katika mchakato mzima wa zabuni na wa utekelezaji wa mkataba. (Untbribery policy code). lililosainiwa na mwombaji mwenyewe.
8. Muombaji/waombaji anatakiwa kuwasilisha picha za Mkurugenzi /Wakurugenzi katika maombi yao
9. Mwombaji ni lazima awe na mtaalamu aliyehitimu katika fani ya afisa afya mazingira, au Afisa afya Mazingira Msaidizi au Msaidizi wa Afya (Environmental Health Officer or Assistant Environmental Health Office or Health assistant) na kivuli cha cheti cha shahada au stashahada cha mtaalam kilichothibitishwa na kamishna wa viapo kiambatanishwe katika maombi.
10. CBOs (vikundi zaidi ya kimoja katika kata wanaweza kushirikiana kutafuta mtaalamu mmoja atakayekuwa mshauri wa vikundi) wa vikundi husika..
11. Waombaji watatakiwa kuonyesha kadi ya gari ya kampuni au mwombaji binafsi Aidha iwapo gari/ mtambo ni wa kukodi muombaji aambatanishe ushahidi wa kisheria wa kukubaliwa kukodishwa na mmiliki
12. Ili kuhakikisha afya na usalama kwa wafanyakazi watatakiwa kupima afya zao mara mbili kwa mwaka na pia wawe na vifaa kinga "personal protective equipments".
13. Kamati ya tathimini itakagua ofisi, magari ya kusafirisha taka, vifaa vya usafi, vielelezo mbali mbali vilivyo tajwa hapo juu katika zoezi la uchambuzi.
14. Mwombaji asiwe na deni lolote analodaiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Iringa. Aidha, mwombaji aliyewahi kushitakiana na Halmashauri ya Manispaa ya Iringa kuhusiana na kazi yeyote, hatapewa nafasi ya ushindani kwa kazi yeyote ya zabuni iliyotangazwa na Halmashauri ya Manispaa ya Iringa. Vile vile mawakala watakaothibitika kuwa na tuhuma za utendaji usiozingatia sheria kutoka taasisi nyingine za Serekali hawatapewa nafasi ya ushindani kwa kazi zinazotangazwa na Halmashauri ya Manispaa ya Iringa.
15. Mwombaji atatakiwa kuthibitisha kisheria kuwa yeye si mtumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa kwa kuambatanisha "affidavit" iliyothibitishwa kisheria.
16. Mwombaji yeyote atakayeshindwa kutimiza au kutokamilisha maelekezo na masharti hayo ya zabuni atakuwa amejiondoa mwenyewe katika ushindani.
17. Halmashauri ya Manispaa ya Iringa hailazimiki kukubali/ kutokubali kutoa zabuni kwa mwombaji kutokana na kigezo cha malipo makubwa au malipo madogo.
18. Zabuni zote zifungwe ndani ya bahasha iliyofungwa kwa lakiri [seal], na juu ya bahasha iandikwe maandishi yanayotaja aina ya zabuni, na namba ya zabuni. Zabuni hizo katika ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Iringa, Kitengo cha Menejimenti ya Ununuzi kwa kutumia Anuani ifuatayo:

    **Mkurugenzi wa Manispaa,**
    **Halmashauri ya Manispaa,**
    **S.L.P. 162, Iringa.**

19. Halmashauri ya Manispaa ya Iringa itafanya kikao cha Kutoa maelezo/ufafanuzi kwaa wazabuni kuhusiana na zabun (Pre bid opening meeting) tarehe 15.09.2022 asubuhi katika ukumbi wa halmashauri ya Manispaa. Waombaji wa zabuni wanasisitizwa kuhudhuria.
20. Kwa maelezo zaidi muombaji anaweza kununua na kusoma nyaraka ya zabuni katika ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa kitengo cha Manunuzi kwa malipo ya **shilingi Hamsini elfu (50,000)** ambazo hazitarudishwa hatakama muombaji hatashinda zabuni. Maombi yaambatane na nakala ya stakabadhi ya malipo.

21 Muda wa mwisho wa kupokea maombi ya zabuni ni **tarehe 19/09/2022 siku ya Jumatatu saa 4:00 asubuhi**. Maombi yote yatafunguliwa mara moja baada ya muda wa mwisho wa uwasiishaji kuwadia. Aidha waombaji au wawakilishi wao wanaalikwa kuhudhuria ufunguzi wa zabuni hizo iwapo watahiari kufanya hivyo.

Maombi yatakayofika baada ya muda uliowekwa kuisha hayatapokelewa hata kwa sababu yoyote.